SEBHA UNIVERSITY JOURNAL OF HUMAN SCIENCES VOL.20 NO. 1 2021
DOI: 10.51984/JOHS.V20I1.1531

جامعة سبها للعلوم الإنسانية مجلة
**Sebha University Journal of Human Sciences**

Journal homepage: https://sebhau.edu.ly/journal/index.php/johs



# Ulinganishi Wa Fonolojia Ya Kiswahili Na Fonolojia Ya Kiarabu

Ibrahim Elhadi Mohamed Lehmedi

Idara Ya Lugha Na Taaluma Za Kiafrika, Kitivu Cha Sanaa, Chuo Kikuu Cha Sebha, Libya

**Keywords:**
Fonolojia
Irabu
Konsonanti
Mfumo
Ulinganishi

**ABSTRACT**

Makala haya yanalenga kulinganisha mifumo ya fonolojia ya lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiarabu. Katika kufanya ulinganishi huu kuna vipengele vitatu vitakavyozingatiwa. Kipengele cha kwanza ni kujadili mfumo wa fonolojia ya Kiarabu. Kipengele cha pili ni kujadili mfumo wa fonolojia ya Kiswahili. Ama katika kipengele cha tatu tutalinganisha kati ya fonolojia ya lugha hizi mbili. Vipengele hivi vitatu ambavyo vitazingatiwa katika utafiti huu vitatoa fununu kubwa juu ya uhusiano na tofauti kati ya fonolojia ya Kiswahili na fonolojia ya Kiarabu;

# مقارنة بين فونولوجيا اللغة السواحيلية واللغة العربية

ابراهيم الهادي محمد لحميدي

قسم اللغات والدراسات الأفريقية، كلية الأداب، جامعة سبها، ليبيا

**الكلمات المفتاحية:**
حروف ساكنة
حروف متحركة
فونولوجيا
مقارنة
نظام

**الملخص**

هذا البحث يهدف لدراسة ومقارنة النظام الفونولوجي للغة العربية واللغة السواحيلية ولتحقيق هذا الهدف تمت مناقشة ثلاثة عناصر اساسية ، العنصر الاول مناقشة النظام الفونولوجي للغة العربية ، ثانيا النظام الفونولوجي للغة السواحيلية ، ثالثا مقارنة للنظام الفونولوجي بين اللغتين. هذه العنتاصر الثلاثة التي تمت مناقشتها في هذا البحث قدمت بيانات وافية عن اوجه الاختلاف والتشابه والعلاقة الفونولوجية بين اللغتين العربية والسواحيلية

## Utangulizi

Katika kamusi ya isimu na lugha (TUKI, 1990: 46) neno fonolojia limefafanuliwa kama tawi la isimu ambalo hushughulikia uchambuzi wa mfumo wa sauti zinazotumiwa katika lugha. Tunaona hapa kuwa fonolojia inaelezwa kama taaluma ambayo kazi yake ni kuchambua mfumo wa sauti zinazotumika katika lugha fulani. Hii inadokeza kwamba kila lugha asilia ina mfumo wake wa sauti. Maelezo haya yana maana kwamba fonolojia inajishughulisha na uchanganuzi wa jinsi sauti za lugha (fulani) zinavyotumika katika kuunda maneno yenye kubeba maana.

Fonolojia ndiyo itakayotuambia ni vipi sauti za lugha fulani zinaundika na vipi zinafanya kazi kama mfumo mmoja. Ni ndani ya eneo la fonolojia ambamo sauti moja inasemekana kutokea au kutotokea katika mfumo wa lugha inayohusika. Fonolojia ya lugha maalumu itatuambia uwezekano tofauti wa miandamano ya sauti katika lugha ile; yaani itatuambia sauti zipi zinaweza kutokea katika mazingira hayo hayo na zipi haziwezi Hyman, L. M. (1975).

### 1- Muhtasari wa Fonolojia ya Kiswahili

Katika kutoa muhtasari wa fonolojia ya Kiswahili ingefaa tuonyeshe na kueleza kwa ufupi idadi ya irabu na konsonanti za Kiswahili sanifu. Yaani kwa maneno mengine ingefaa tuonyeshe orodha ya sauti zote za lugha hii, namna zinavyotamkwa, na mahali zinapotamkiwa. Aidha tutaeleza pia jinsi sauti hizi mbalimbali zinavyotumika katika kuunda maneno ya lugha ya Kiswahili.

### 1.1 Irabu za Kiswahili Sanifu

**Maana ya irabu ni aina ya sauti za lugha ambazo hutamkwa bila kuwepo na kizuizi chochote kwenye mkondo wa hewa utokao mapafuni ukipita katika chemba ya kinywa na chemba ya pua kwenda nje (taz. Alaam, A. & Rabii, A.1988 : 154; Kihore na wenzie 2001: 19).Katika lugha ya Kiswahili inaonekana kwamba irabu za Kiswahili sanifu ni tano, yaani [a], [e], [i], [o] na [u] nazo zimeonyeshwa katika jedwali lifuatalo. Alama za kifonetiki zilizotumika ni zile ambazo zimependekezwa na IPA (International**

*Corresponding author:
E-mail addresses: ibr.lehmedi@sebhau.edu.ly
*Article History : Received 12 April 2021 - Received in revised form 23 June 2021 - Accepted 30 June 2021*

**Phonetic Association). Kwa desturi irabu hizi huwa ni fupi kimaandishi. Kwa mujibu wa maelezo ya Kihore na wenzie (2001) tunaweza kuzieleza irabu hizi kwa kutumia Jedwali lifuatalo:**

| Sauti | Kifonetiki | Mfano | Kifonetiki |
|---|---|---|---|
| A | [ a ] | pata | [pata] |
| E | [ ɛ ] | embe | [ɛmbɛ] |
| I | [ i ] | dini | [dini] |
| O | [Ɔ ] | moto | [mƆtƆ] |
| U | [ u ] | nuru | [nuru] |

*Irabu za Kiswahili sanifu*

### 1.2 Konsonanti za Kiswahili Sanifu

**Konsonanti ni aina ya sauti ambazo hutamkwa kwa kuzuia mkondo hewa kutoka mapafuni, ukipita chemba ya kinywa na chemba ya pua kwaenda nje.Lugha ya Kiswahili inazo sauti za konsonanti ishirini na tano. Kihore na wenzie (2001: 23) wanasema kwamba Kiswahili kina konsonanti ishirini na tatu na viyeyusho viwili na kwamba viyeyusho hivyo havihesabiki kama konsonanti halisi.**

## 2- Muhtasari wa Fonolojia ya Kiarabu

**Ni muhimu sana kutoa maelezo mafupi kuhusu idadi ya irabu na konsonanti za Kiarabu Kama tulivyofanya kwa upande wa lugha ya Kiswahili hapa juu.**

Lugha ya Kiarabu ni lugha iliyomo katika kundi kubwa la lugha za Kisemiti. Kihistoria lugha hii inaundwa na matawi mawili nayo ni: Kiarabu cha Kusini na Kiarabu cha Kaskazini (taz. Salman, H. 1970: 82). Lugha ya Kiarabu inatumika katika nchi zote za Kiarabu; lugha hii pia ni lugha ya sayansi na lugha ya kufundishia.

Lugha ya Kiarabu kama lugha nyingine ulimwenguni imejengwa na sauti. Katika sehemu ifuatayo tutajaribu kuonyesha aina za sauti zilizomo katika lugha ya Kiarabu.

### 2.1 Irabu za Kiarabu Sanifu

Alaam, A. & Rabii, A. 1988: 154) wanadai kwamba Lugha ya Kiarabu sanifu ina irabu sita. Irabu hizi zinagawanyika katika makundi mawili, yaani tatu ni fupi na tatu nyingine ni ndefu. Irabu za kundi la kwanza ni *Al fatha*, *Al kasra* na *Al dhamma*. Tunaweza kuzifafanua irabu hizi kama ifuatayo (Irabu zinazohusika zimepigiwa mistari ):

**(a) *Al fatha* (الفتحة ):** Inawakilisha irabu [a] kwa mfano sauti [ مَ ] ma (wazi) inaitwa hivyo kutokana na uwazi wa njia ya mkondohewa utokao ndani ya mapafu kwenda nje. Kistari kifupi kilichowekwa juu ya herufi badala ya [a], huitwa *Al fatha*. Mfano wa irabu hii ni kama ifuatayo:

**Kifonetiki Kiara maana ktka Kiswa**
[rasama] [ رسم ] alichora

**(b) *Al kasra* (الكسرة) :** Inawakilisha irabu [i] kwa mfano sauti [ مِ ] mi (kupanguka) sauti hii inaitwa hivyo kwa sababu mkondohewa hupanguliwa kidogo na mkao wa ulimi ambao unafanya njia iwe nyembamba na midomo kuwa kama inataka kukaribiana. Kistari kifupi kilichowekwa chini ya herufi badala ya [i], huitwa *Al kasra* Bosha, I. (1994). Mfano wa irabu hii ni kama ifuatayo:

**Kifonetiki Kiara maana ktka Kiswa**
[mifta:h] [ مفتاح ] ufunguo

**(ch) *Al dhamma* (الظمة ) :** Inawakilisha irabu [u] kwa mfano sauti [ مُ ] mu (kujikusanya pamoja) sauti hii inaashiria mkao wa midomo. Alama kama koma ( ’ ) iliyo juu ya herufi badala ya [u], huitwa *Al dhamma* Chunguza mifano ifuatayo:

**Kifonetiki Kiarabu maana katika Kiswahili**
[mudaris] [ مدرس ] mwalimu

Irabu hizo fupi tatu zinafanya kazi kubwa katika lugha ya Kiarabu. Irabu katika matumizi yake zinaweza kabisa kubadilisha maana za maneno. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:

**Kifonetiki Kiara maana ktka Kiswa**
[kafr] [كفر ] kijiji
[kufr] [ كفر ] ukafiri
[kifr] [ كفر ] ardhi kame

**Tanbihi**: Ingefaa tukumbushe kwamba katika lugha ya Kiarabu kuna alama mbili ambazo zinaitwa *Al sukun* na *Al shadda*. (Mwansoko 1995 )

***Al sukun* ( o ):** Ni alama ionyeshayo kutokuwepo kwa vokali. Kwa mfano:

**Kifonetiki Kiara Maana ktka Kiswa**
[shahr] شهر mwezi
[hajar] حجر jiwe

***Al shadda* ( ):** Ni alama ionyeshayo kuradidi konsonanti. Kwa mfano:

**Kifonetiki Kiara Maana ktka Kiswa**
[fassr] فسر amefasiri
[ɟadda] جدة bibi

Irabu za kundi la pili ni *Al alif*, *Al waaw* na *Al yaa*. Irabu hizi zasemekana kuwa ndefu kwa sababu zinachukua muda mrefu zaidi kutamkwa kuliko zile fupi. Irabu hizi huchukuliwa na wanaisimu wa lugha ya Kiarabu kuwa herufi za urefushaji. Katika lugha ya Kiarabu zinajulikana kama *Al mad* (taz.Gairdener, w. H. 1925: 34). Chunguza kwa makini mifano ifuatayo (irabu zinazohusika zimepigiwa mistari):

**(i) *Al alif* ( ا )** : Inawakilisha irabu [a:] yaani irabu ya matokeo ya urefushaji wa irabu [a], kwa mfano, [ مـا ] ma: . Mfano wake ni kama ifuatayo:

**Kifonetiki Kiara maana ktka Kiswa**
[sa:riq] [ سارق ] mwizi

**(ii) *Al waaw* ( و ):** Inawakilisha irabu [u:] yaani irabu ya matokeo ya urefushaji wa irabu [u], kama, [ مو ] mu: . Tuangalie mfano huu:

**Kifonetiki Kiara maana ktka Kiswa**
[qu:l] [ قول ] usemi

**(iii) *Al yaa* ( ي ):** Inawakilisha irabu [i:] yaani irabu ya matokeo ya urefushaji wa irabu [i], kama, [ مي ] mi: . Tuangalie mfano huu:

**Kifonetiki Kiara maana ktka Kiswa**
[bi:t] [ بيت ] nyumba (umoja)

Irabu hizi nazo, kama zilivyo irabu fupi, huweza kubadili maana za maneno. Tutazame mifano hii :

**Kifonetiki Kiara maana ktka Kiswa**
[na:r] [ نار ] moto
[nu:r] [ نور ] mwangaza

Kwa upande wa uamilifu *Al fatha*, *Al kasra* na *Al dhamma* hufanya kazi tofauti na *Al alif*, *Al waaw* na *Al yaa*. Angalia mifano hii :
Tofauti kati ya [a] na [a:]: Tofauti kati ya *Al fatha* na *Al alif* kikazi ni kwamba *Al fatha* inafanya kazi ya njeo ya wakati uliopita. Ama kuhusu *Al alif* inafanya kazi ya ushirikiano wa utendaji wa tendo katika njeo ya wakati uliopita. Hebu tutazame mifano ifuatayo:

**Kifonetiki Kiara maana ktka Kiswa**
[ʈalaba] [ طلب ] ameomba
[ʈa:laba] [ طالب ] amedai

Tofauti baina ya [u] na [u:]: Tofauti kati ya *Al dhamma* na *Al waaw* kikazi ni kwamba *Al dhamma* inafanya kazi ya njeo ya wakati uliopita. Ama kuhusu *Al waaw* inafanya kazi ya kushirikisha mtendwa katika tendo katika njeo ya wakati uliopita. Hebu tutazame mifano ifuatayo:

**Kifonetiki Kiar maana ktka Kiswa**
[kutiba] [ كتب ] imeandikwa
[ʈu:liba] [ طولب ] amedaiwa

Tofauti baina ya [i] na [i:]: Tofauti kati ya *Al kasra* na *Al yaa* kikazi ni kwamba *Al kasra* inafanya kazi ya njeo ya wakati uliopita. *Al yaa* inafanya kazi ya kivumishi. Hebu tutazame mifano ifuatayo:

**Kifonetiki Kiar maana ktka Kiswa**
[raħima] [ رحم ] amerehemu
[raħi:m] [ رحيم ] mwenye kurehemu

### 2.2 Konsonanti za Kiarabu Sanifu

Kutokana na kuangalia mfumo wa sauti katika lugha ya Kiarabu sanifu tunakuta kwamba Kiarabu sanifu kina konsonanti ishirini na nane (28). Kwa baadhi ya wanazuoni wa lugha ya Kiarabu sauti [w, y] huhesabika kama konsonanti kamili (taz. Barkawi: 126); lakini baadhi yao wana maoni kwamba [w, y] si konsonanti bali ni nusu-irabu (taz. Gairdner 1925: 32; Bishr, K. 1975 ). Jedwali lifuatalo linaonyesha sauti za konsonanti hizi:

| KIFONETIKI | SAUTI KWA KIRUMI | SAUTI KWA KIARABU | Matamshi YA NENO KIFONETIKI | MAANDISHI KATIKA KIARABU | MAANA KATIKA KISWAHILI |
|---|---|---|---|---|---|
| [ b ] | B | ب | [ba:b] | باب | mlango |
| [ t ] | T | ت | [taqdi:r] | تقدير | kadirio |
| [ θ ] | Th | ث | [θawa:b] | ثواب | thawabu |
| [ ɟ ] | J | ج | [ɟa:su:s] | جاسوس | jasusi |
| [ ħ ] | Ħ | ح | [ħuɟɟa] | حجة | hoja |
| [ x ] | Kh | خ | [xuŧba] | خطبة | hotuba |
| [ d ] | D | د | [dam] | دم | damu |
| [ ð ] | Đ | ذ | [ða:t] | ذا ت | dhati |
| [r ] | R | ر | [rifqa] | رفقة | urafiki |
| [ z ] | Z | ز | [zama:n] | زمان | zamani |
| [ s ] | S | س | [sama:d] | سماد | mbolea |
| [ ʃ ] | Sh | ش | [ʃaħm] | شحم | shahamu |
| [ š ] | Š | ص | [šanm] | صنم | sanamu |
| [ đ ] | Đ | ض | [đid] | ظد | dhidhi |
| [ ŧ ] | Ŧ | ط | [ŧabaqa] | طبقة | tabaka |
| [ ƶ ] | Ƶ | ظ | [ƶa:lim] | ظالم | dhalimu |
| [ ˤ ] | ˤ | ع | [ˤ ilm] | علم | ilimu |
| [ γ ] | Gh | غ | [γara:ma] | غرا مة | gharama |
| [ f ] | F | ف | [faħal] | فحل | fahali |
| [ q ] | Q | ق | [qa:nu:n] | قانون | kanuni |
| [ k ] | K | ك | [kafan] | كفن | sanda |
| [ l ] | L | ل | [li:wna] | ليونة | ulaini |
| [ m ] | M | م | [muʃa:raka] | مشاركة | ushirikiano |
| [ n ] | N | ن | [na:r] | نار | moto |
| ;[ h ] | H | ه | [ha:ti:f] | هاتف | simu |
| [ w ] | W | و | [wald] | ولد | mtoto |
| [ y ] | Y | ى | [ya:qu:t] | ياقوت | yakuti |
| [ ? ] | ? | ء | [?iðaˤa] | اذاعة | idhaa |

*Konsonanti za Kiarabu Sanifu*

**Tumekwishaona kwamba lugha ya Kiarabu ina konsonanti ishirini na nane, na sasa tutajaribu kutoa maelezo mafupi kuhusu sauti hizi kama zinavyojitokeza katika Jedwalli la juu.**

**3. Ulinganishi wa Mfumo wa Konsonanti za Kiswahili na za Kiarabu**

Katika Sehemu ( taz. Maelezo 1.2 na 2.2 ) hapo juu tulionyesha mfumo wa konsonanti za Kiswahili na za Kiarabu.

Kama tulivyosema lugha ya Kiswahili ina konsonanti ishrini na tao na viyeyusho viwili ambazo ni [ b, d, g, p, t, k, ɟ, ʃ, tʃ, ŋ, ɲ, v, ð, z, f, h, γ, θ, s, l, m, n, r, w, y ], wakati lugha ya Kiarabu ina konsonanti ishirini na nane ambazo ni [ b, d, t, ŧ, k, q, ?, đ, ɟ, f, θ, s, š, ʃ, x, ħ, h, ð, ƶ, z, r, ˤ, l, m, n, γ, w, y ].

Kutokana na orodha hizi mbili za sauti tunaona kwamba baadhi ya konsonanti zimo katika lugha zote mbili na baadhi zimo katika lugha ya Kiarabu lakini hazimo katika lugha ya Kiswahili. Halikadhalika baadhi ya konsonanti zimo katika lugha ya Kiswahili lakini hazimo katika lugha ya Kiarabu. Ibrahim, E.M. (2004),

Ili tuweze kulinganisha na kupambanua mifumo ya konsonanti za lugha hizi mbili ingefaa tuzigawanye konsonanti hizi katika makundi matatu; yaani:

1. Kundi la konsonanti ambazo zimo katika lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiarabu.
2. Kundi la konsonanti ambazo zimo katika lugha ya Kiarabu lakini hazimo katika lugha ya Kiswahili.
3. Kundi la konsonanti ambazo zimo katika lugha ya Kiswahili lakini hazimo katika lugha ya Kiarabu.

**3.1 Konsonanti ambazo zimo katika lugha ya Kiswahili na lugha ya Kiarabu**

Katika kundi hili kuna konsonanti kumi na tisa ambazo zimo katika lugha zote mbili, nazo ni [ b, d, t, k, ɟ, ʃ, ð, z, f, h, γ, θ, s, l, m, n, r, w, y ]. Ijapokuwa konsonanti hizi zinafanana katika jinsi na mahali pa matamshi lakini si rupia kwa nyenziye katika lugha zote mbili.

Inaonekana wazi kwamba lugha ya Kiswahili ina konsonanti (19) ambazo zinafanana na zile zilizomo katika lugha ya Kiarabu. Lakini kama tulivyoeleza katika aya iliyotangulia hatuwezi kusema kwamba konsonanti hizo ni rupia kwa nyenziye katika lugha zote mbili kwa sababu zifuatazo:

1. Katika lugha ya Kiarabu konsonanti ghuna (kama vile *d*, *b*, *z*) zinakuwa na mrindimo mkubwa zaidi mwanzoni mwa neno kuliko ilivyo katika Kiswahili.
2. Katika lugha ya Kiarabu zile sauti zisizobadilika na ambazo zinatamkiwa kwenye ncha ya ulimi karibu na meno ya mbele kama [t, d, n] siku zote hutamkwa kwa kukandamiza ncha ya ulimi kwa nguvu nyuma ya meno ya mbele ya juu.
3. “ r “ ya Kiarabu hutamkwa kwa nguvu zaidi kuliko “ r “ ya Kiswahili. Inatamkwa kwa kugonga haraka ncha ya ulimi nyuma ya ufizi wa meno ya mbele ya juu , na wakati huo huo kukiwa na mpumo. Inakaribiana sana na “ r “ ya Kiingereza cha Ireland katika matamshi ya maneno “ very “ na “ merry “.

**3.2 Konsonanti ambazo zimo katika Kiswahili lakini hazimo katika Kiarabu**

Konsonanti sita (6) za Kiswahili ambazo hazina visawe katika lugha ya Kiarabu, sauti hizo ni [p, g, v, tʃ, ŋ, ɲ]. Hebu tuangalie na tuchunguze sauti hizo sita pamoja na mifano yake:

Sauti [p**]:** hii hutamkwa kwa kuikutanisha midomo miwili. Sauti hii ni ya kipasuo kisichoghuna. Tukiangalia mfumo wa konsonanti za lugha ya Kiarabu tutaona kwamba sauti hii haimo. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:

| Kifonetiki | Kiswa | Matamshi ya Kiar |
|---|---|---|
| [pƆle] | pole | *[buli] |
| [alinip] | alinipa | *[aliniba] |
| [pia] | pia | *[bia] |

**Sauti [g]:** ni ya kipasuo ghuna ambacho hutamkiwa kwenye kaakaa laini. Katika mfumo wa konsonanti za Kiarabu sanifu sauti hii haimo [ingawa katika matamshi ya kienyeji inawezekana kutamka hivyo]. Hebu tuangalie mifano haya ifuatayo:

| Kifonetiki | Kiswa | Matamshi ya Kiar |
|---|---|---|
| [gani] | gani | [gani] |

[mbƆga] mboga [mbuga]
[inatɛgɛmea] inategemea [inatigimia]

**Sauti [v]:** hii hutamkwa wakati mdomo wa chini unapokuwa umeguswa na meno ya juu, Sauti hii ni kikwamizwa ghuna. Sauti hii haina kisawe chake katika lugha ya Kiarabu. Waarabu wanaitamka sauti hii mara nyingi kwa kutumia sauti [f]. Tutazame mifano ifuatayo:

| **Kifonetiki** | **Kiswa** | **Matamshi ya Kiar** |
|---|---|---|
| [viwanda] | viwanda | *[fiwanda] |
| [mvua] | mvua | *[mfua] |
| [vua] | vua | *[fua] |

**Sauti [tʃ] :** hii ni ya kaakaa gumu, na ambayo ni kizuio – kwamiza. Sauti hii haimo katika lugha ya Kiarabu, Waarabu mara nyingi huitamka sauti hii kama sauti [ʃ]. Tutazame mifano haya ifuatayo:

| **Kifonetiki** | **Kiswa** | **Matamshi ya Kiar** |
|---|---|---|
| [tʃumba] | chumba | *[shumba] |
| [mtʃaŋga] | mchanga | *[mshaŋga] |
| [tʃɛmʃa] | chemsha | *[shimsha] |

**Sauti [ŋ]:** hii ni nazali ya kaakaa laini. Hutamkwa kwa kuruhusu hewa itakayo mapafuni ipitie katika chemba ya pua. Sauti hii haina kisawe katika lugha ya Kiarabu mara nyingi wanaitamka kama [ng]. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:

| **Kifonetiki** | **Kiswa** | **Matamshi ya Kiar** |
|---|---|---|
| [ŋƆmbɛ] | ng'ombe | *[ŋgumbi] |
| [ŋaŋania] | ng'ang'ania | *[ŋgaŋgania] |
| [ŋanda] | ng'anda | *[ŋganda] |

**Sauti [ɲ]:** hii ni nazali inayofanana sana sauti [ŋ] sauti hii hutamkwa kwa kukutanisha ulimi na kaakaa-gumu. Vile vile sauti hii haina kisawe katika lugha ya Kiarabu. Ijapokuwa sauti hii haina kisawe lakini wanafunzi wa Kiarabu wanaweza kuitamka sawasawa. Hebu tutazame mifano ifuatayo:

| **Kifonetiki** | **Kisw** | **Matamshi ya Kiar** |
|---|---|---|
| [ɲaɲa] | nyanya | [ɲaɲa] |
| [ɲɛʃa] | nyesha | [ɲisha] |
| [ɲama] | nyama | [ɲama] |

**Tanbihi:** * hii ina maana ya jinsi ya kutamka itumiwayo na wazungumzaji wa Kiarabu.

### 3.3 Konsonanti ambazo zimo katika lugha ya Kiarabu lakini hazimo katika lugha ya Kiswahili

Konsonanti ambazo zimo katika lugha ya Kiarabu lakini hazimo katika lugha ya Kiswahili ni tisa (9) nazo ni [ q, x, ħ, ʕ, ?, ŧ, đ, ẓ, š ]. Hii ni kusema kwamba konsonanti hizo tisa za Kiarabu hazina visawe katika lugha ya Kiswahili.

Yafaa kuzifafanua konsonanti hizo kwa makini zaidi. Hebu tuangalie konsonanti hizi pamoja na mifano yake:

**[q] [ ق ]:** Sauti hii ni kizuio cha kidakatonge. Hii ni konsonanti nzito na hutamkiwa kooni kwa kuiweka sehemu ya nyuma ya ulimi kwenye ukuta wa koo. Hebu tuangalie mifano; ifuatayo:

| **Kifonetiki** | **Kiara** | **Maana katika Kisw** |
|---|---|---|
| [qamar] | قمر | mwezi |

***** Sauti hii ni ngumu kwa wageni ambao wanataka kujifunza Kiarabu. Inatamkika kwa urahisi tu kwa watu ambao wameshajifunza au wametumia Kiarabu toka utoto wao (taz. Rawhia 1984: 130 – 131).

**[x] [ خ ] :** Sauti hii ni kizuio kiwamiza ambacho hutamkiwa nyuma kabisa ya kinywa; ni kifulizwa cha kidakatonge kisichoghuna. Tuangalie mifano ifuatayo:

| **Kfonetiki** | **Kiarabu** | **Maana ktk Kisw** |
|---|---|---|
| [xabar] | خبر | habari |

**Tanbihi:** * sauti hii ilikuwa inatumika zamani katika lugha ya Kiswahili na inakuwa inatumika sana na Wazanzibari kwa mfano: khabari , kheri n.k.

**[ħ] [ح]:** Sauti hii ni kikwamizwa kisichoghuna cha koromeo. Ni sauti yenye nguvu lakini; laini itokayo kifuani na ambayo hutamkwa kwa kulazimisha hewa kupita katikati ya glota ambayo huwa karibu imefunga, kama inavyotokea unaposhusha pumzi kwa nguvu. Tunaweza kusema kwamba sauti hii ni sawa na [h] ya Kiswahili ambayo imeongezewa mpumuo. Hebu Tutazame mifano ifuatayo:

| **Kifonetiki** | **Kiarabu** | **Maana ktk Kisw** |
|---|---|---|
| [ħaqi:qa] | حقيقة | hakika |

**[ ʕ ] [ ع ] :** Hii ni sauti kali ya kooni itamkwayo kwa kutoa pumzi na wakati huo huo ukiwa unalifunga koo kwa haraka na nguvu, kama katika mifano ifuatayo:

| **Kifonetiki** | **Kiarabu** | **Maana ktk Kisw** |
|---|---|---|
| [ʕarabi:] | عربى | Mwarabu |

**[?] [ ء ]:** Sauti hii ni kipasuo kisichobadilika ambacho hutamkwa kwa kufunga nyuzisauti na kisha kuzifungua ghafla. Mara nyingi hujulikana kama " kizuio cha glota kisichoghuna " kutokana na namna ya utamkaji wake, kwa maana kwamba hakiwezi kutolewa kwa mpasuo na wakati huo huo nyuzisauti zikiwa zinarindima. Sauti [?] katika Kiarabu inajulikana kama *Al hamza*. Tutazame mifano ifuatayo:

| **Kifonetiki** | **Kiarabu** | **Maana ktk Kisw** |
|---|---|---|
| [?alam] | ألم | maumivu |

**[ ŧ, đ, ẓ, š ] ( ط ، ض ، ظ ، ص ) (Visisitizi):** Mbali na sauti hizo zisizobadilifu kuna nne nyingine ambazo nazo husababisha matatizo ya kimatamshi kwa wazungumzaji wasio wazawa wa Kiarabu. Sauti hizi mara nyingi huandikwa kama sauti za Kiswahili [t], [d], [ð ] na [s] lakini zinaitwa visisitizi visivyobadilifu; yaani vitamkwa hivi kila mara vinaonyesha hali ya kusisitiza. Katika utamkaji wake utaratibu utumikao ni kama ule wa kutamka [t], [d], [ð] na [s] isipokuwa nyuma ya ulimi huwa kumeinuliwa kuelekea kwenye kaakaa laini. Mkao huo wa ulimi huzipa sauti hizi aina fulani ya uzito ambao hujitokeza kama msisitizo wa namna fulani ambao huzitofautisha na sauti nyenziye za Kiswahili. Hebu tuangalie mifano ifuatayo:

| **Kifonetiki** | **Kiarabu** | **Maana ktk Kisw** |
|---|---|---|
| [ŧa:lib] | طالب | mwanafunzi |
| [đami:r] | ضمير | dhamira |
| [bašal] | بصل | vitunguu |

### 4. Ulinganishi wa Mfumo wa Irabu za Kiswahili na Irabu za Kiarabu

Katika Sehemu ( taz. Maelezo 1.1 na 2.1 ) hapo juu tulionyesha mfumo wa Irabu za Kiswahili na za Kiarabu.

Kuna irabu tano (5) Katika lugha ya Kiswahili ambazo ni *a*, *e*, *i*, *o*, na *u*. Irabu hizi ni fupi katika utamkaji wake. Lugha ya Kiarabu ina irabu sita (6) ambazo zimegawanyika katika makundi mawili, yaani irabu fupi na irabu ndefu. Irabu fupi ni *Al fatha*, *Al kasra* na *Al dhama*. Katika lugha ya Kiarabu irabu fupi zinawakilishwa kwa alama zinazoitwa "*harak*a" yaani *Al fatha* [a] , *Al kasra* [i] na *Al dhamma* [u].

Irabu ndefu ni tatu nazo ni *Al alif* [a:] [ ا ], *Al waaw* [u:] [ و ] na *Al yaa* [i:] [ ى ].

Kutokana na maelezo ( 1.1 na 2.1 ) hayo tunaona kwamba lugha ya Kiswahili inazo irabu tano wakati lugha ya Kiarabu inazo irabu sita. Ingawa kuna baadhi ya wanazuoni (Massamba, 1987 mazungumzo yake) wanadai kwamba hata katika lugha ya Kiswahili kuna irabu ndefu.

**Irabu [a]** imo katika lugha zote mbili, sauti hii hutamkiwa kwa chini katika lugha zote mbili

| **[a] ya Kiarabu** | **[a] ya Kiswahili** |
|---|---|
| _ juu | _ juu |
| _ mbele | _ mbele |
| _ nyuma | _ nyuma |

**Irabu [i]** vile vile imo katika lugha zote mbili, sauti hii hutamkiwa kwa mbele na juu katika lugha zote mbili.

| **[ i ] ya Kiarabu** | **[ i ] ya Kiswahili** |
|---|---|
| + juu | + juu |
| + mbele | + mbele |
| _ nyuma | _ nyuma |

**Irabu [u]** halikadhalika imo katika lugha hizi mbili, sauti hii

hutamkiwa kwa juu na nyuma katika lugha zote mbili.

| **[ u ] ya Kiarabu** | **[ u ] ya Kiswahili** |
|---|---|
| + juu | + juu |
| + nyuma | + nyuma |

**Irabu [e]** hii ni ya mbele na katikati, inafanana kidogo na irabu [i]. Mifano ya irabu hii ni kama ifutayo:

| **Kifonetiki** | **Kiswahili** |
|---|---|
| [pɛnda] | penda |

**Irabu [o]** hii ni ya nyuma na katikati, inafanana kidogo na irabu [u]. Mifano ya irabu hii ni kama ifuatayo:

| **Kifonetiki** | **Kiswahili** |
|---|---|
| [sƆkƆ] | soko |

## 5. HITIMISHO

Kutokana na tarifa zilizotolewa na zilizochuguzwa katika makala hii ya kulinganisha na kulinganua mifomu ya fonolojia ya lugha ya Kiswahili na ya Kiarabu matokeo yalikuwa wazi kwamba:

1- Kuna konsonanti kumi na tisa ambazo zimo katika lugha zote mbili, nazo ni [ b, d, t, k, ɟ, ʃ, ð, z, f, h, γ, θ, s, l, m, n, r, w, y ]. Ijapokuwa konsonanti hizi zinafanana katika jinsi na mahali pa matamshi lakini si rupia kwa nyenziye katika lugha zote mbili.

2- Konsonanti sita (6) za Kiswahili ambazo hazina visawe katika lugha ya Kiarabu, sauti hizo ni [p, g, v, tʃ, ŋ, ɲ].

3- Konsonanti ambazo zimo katika lugha ya Kiarabu lakini hazimo katika lugha ya Kiswahili ni tisa (9) nazo ni [ q, x, ħ, ʕ, ?, ƚ, đ, ẓ, š ]. Hii ni kusema kwamba konsonanti hizo tisa za Kiarabu hazina visawe katika lugha ya Kiswahili.

4- Kuna irabu tano (5) Katika lugha ya Kiswahili ambazo ni *a*, *e*, *i*, *o*, na *u*. Irabu hizi ni fupi katika utamkaji wake.

5- Lugha ya Kiarabu ina irabu sita (6) ambazo zimegawanyika katika makundi mawili, yaani irabu fupi na irabu ndefu. Irabu fupi ni *Al fatha*, *Al kasra* na *Al dhama*. Katika lugha ya Kiarabu irabu fupi zinawakilishwa kwa alama zinazoitwa "*harak*a" yaani *Al fatha* [a] , *Al kasra* [i] na *Al dhamma* [u]. Irabu ndefu ni tatu nazo ni *Al alif* [a:] [ ا ], *Al waaw* [u:] [ و ] na *Al yaa* [i:] [ ى ].

## MAREJEO


[1] Alaam, A. A. & Rabii, A. (1988) عبدالعزيز احمد علام و عبدالله ربيع *علم الصوتيات* مكتبة الطالب الجامعى، الطبعة التانية مكة المكرمة.

[2] Barkawi, A. (1984) عبدالفتاح البركاوى *مقدمة فى اصوات اللغة* مؤسسة الرسالة الطبعة التالتة

[3] Bishr, K. (1975) كمال *علم اللغة العام – الأصوات* الطبعة الرابعة بشر

[4] Bosha, I. (1994) Athari za Kiarabu katika Kiswahili sanifu. M.A Dissertaion. University of Dar es salaam.

[5] Guthrie, M. (1967) *Comparative Bantu* Vlo.1 : An Introduction to the comparative Linguistics and Prehistoryof the Bantu Languages. Farnborough :Gregg

[6] Hyman, L. M. (1975) *Phonology: theory and analysis*, Holt, Rinehart & Winston

[7] Ibrahim, E.M. (2004), Matatizo Ya Matamshi Wanayowapata Wanafunzi Wa Kiarabu Wanapojifunza Kiswahili Sanifu. Tasnifu ya digirii Ya Uzamili ya M.A.(KiKiswahili) Katika Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Dar es Salaam.

[8] IPA (1981) *International Alphonetic Association*, University college, gower street, London WCIE 6BT.

[9] Kihore ,Y.M. (na wenzie) (2001) *Sarufi Maumbo ya Kiswahili sanifu* , TUKI

[10] Massamba, D.P.B. (1987) "The Effect of Language Modernization on the Phonological System of the Kiswahili Language." *Kiswahili Juzuu* 54/1 & 54/2

[11] Mwanasoko (1995) "Shadda katika Kiswahili" *Kioo cha Lugha Juzuu 1*, Na.1 uk.15-19

[12] Rawhia, K. (1984) *The problems encountered by English speakers in learning Arabic*. General publication of distribution company Tripoli.

[13] Salman, H. A. (1970) *Arabic fonology*, Indiana University. Mouton The Hague-Paris

[14] TUKI (1990) *Kamusi sanifu ya isimu na lugha*. DUP. Dar es salaamkeywords)